# JARIBIO LA MTIHANI WA SHULE
# DARASA LA SABA - MWAKA 2021
# KISWAHILI : LUGHA

SASON 007

7

***JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU*** **MUDA: SAA1 DAK.40**

1. *Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina Maswali 50*
2. *Hakikisha umeandika:-*
   *(i) JINA LAKO* *(ii) JINA LA SHULE YAKO*
3. *Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali*

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15 . Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo chini. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Masomo ___1___ msingi ___2___ mfululizo ___3___ masomo ya Kiswahili ___4___ darasa la kwanza ___5___ la nane. Kila kitabu kimegawanywa katika hatua tatu, kila hatua ikijiunga ___6___ ___7___ kulingana na mfulizo huo. Kulingana na kazi, hatua inapaswa kazi ya ___8___ ___9___ .

Masomo ya msingi kitabu cha nne kimedhaminiwa kutumiwa na watoto wa darasa la nane. Kitabu ___10___ ni toleo jipya.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. ya | B. za | C. vya | D. ni |
| 2. | A. na | B. kwa | C. ni | D. za |
| 3. | A. kwa | B. wa | C. za | D. vya |
| 4. | A. na | B. tokea | C. mpaka | D. taka |
| 5. | A. kwanza | B. handi | C. hadi | D. mwanzo |
| 6. | A. ni | B. na | C. katika | D. ndeni |
| 7. | A. nyingine | B. nyingi | C. vingi | D. kwingi |
| 8. | A. mhule | B. muhula | C. mihula | D. viula |
| 9. | A. mmoja | B. moja | C. namoja | D. moja |
| 10. | A. hivi | B. iki | C. hiki | D. hicho |

Tindi alijua kwamba anahitaji kutia bidii masomoni asije ___11___ shule. Kijijini mwao kulikuwa kawaida wasichana ___12___ nafasi katika elimu. Palipotokea uhaba ___13___ karo, masomo ya msichana ___14___ huku mvulana akiendelea na elimu mara hii Tindi aliamua kutia bidii ili angalau mwalimu mkuu amtafutie mhisani ___15___.


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. | A. akaachishwa | B. akaachiwa | C. akaachilia | D. akaachia |
| 12. | A. kunyanyaswa | B. kuhadilishwa | C. kudhulumiwa | D. kupunguziwa |
| 13. | A. ya | B. kwa | C. wa | D. na |
| 14. | A. yangekatizwa | B. yanaketizwa | C. yakikatizwa | D. yakaketizwa |
| 15. | A. agethadhamini masomo yake | B. amthamini masomo yake | C. amdhamini masomo yake | D. ayadhamini masomo yake |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi;***

16. Jana usiku nilishuhudia __________ ya nyota.
A. mwangaza B. thureya
C. kundi D. kumetameta

17. Aliuficha mkate __________.
A. kabatini B. kwenye kabatini
C. kabati D. katika kabatini

18. Umbo lifuatalo laitwaje?



A. kia B. pembe tatu
C. pia D. moyo

19. Mtoto wa papa huitwaje?
A. Kiluwiluwi B. Kinengwe
C. Kiwavi D. Kisase

20. Sehemu inayopatikana kwenye kichwa ni ___
A. kwapa B. kisigino
C. kope D. kisugudi

21. ***Andika kinyume cha sentensi hii:-***
Kijana mwembamba anaenda.
A. Msichana mrefu anakuja.
B. Msichana mnene anakuja.
C. Mzee mnene haji.
D. Mzee mnene anakuja.

22. Chagua sentensi iliyo katika hali ya ***kutendana***
A. Yohana walivutana na Matata kwa kamba
B. Yohana na Matata walivutana kwa kamba
C. Matata alivutwa kwa kamba na Yohana
D. Matata alivutika kwa kamba na Yohana

23. ***Tumia -enye vizuri kukamilisha sentensi:-***
Shamba __________ miwa limelimwa.
A. wenye B. kwenye
C. lenye D. lenyewe

24. Kiziwa __________ kidonda amepelekwa hospitali.
A. chenyewe B. mwenyewe
C. chenye D. mwenye

25. ***Tumia o-ote kukamilisha sentensi:-***
Mvulana __________ anahitajika.
A. yoyote B. wowote
C. yeyote D. wote

26. Gari __________ litasimamishwa.
A. lolote B. zote
C. zozote D. wote

27. Chagua jibu sahihi linaloonyesha kundi la vitenzi pekee
A. Huyu, hiki, hawa, hizo
B. Yangu, kwake, chetu, lako
C. Mlango, gari, kalamu, mtoto
D. Piga, cheka, imba, tembea

28. Taja majina ya akisami zifuatazo
$^1/_4$, $^1/_6$, $^1/_9$, $^1/_5$
A. Robo, thumni, subui, sudusi
B. Robo, sudusi, tusui, humusi
C. Robo, tusui, sudusi, thumni
D. Robo, thuluthi, tusui, thumni

29. ***Ni ufupisho upi ulio sahihi:-***
Baba yake
A. babaye B. babake
C. babako D. babayo

30. ***Kanusha:-***
Moto umewaka leo
A. Moto haukuwaka leo
B. Moto haujawaka leo
C. Moto hautawaka leo
D. Moto hauwaki leo

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40**

"Mkuu wa elimu, mwalimu mkuu wa shule hii. Kinara wa kamati ya shule wanariadha wakufunzi wapendwa, mabibi na mabwana masalkheri?

Leo ninayo furaha mpwitompwito kusimama kidete kidam ili kuwasheheneza shukrani chungu nzima wanariadha wetu kwa kujitolea mhanga kuipeperusha bendera ya shule yetu.

Kwanza, michezo ya riadha ina faida anuwai, mathalan mwanariadha hujikatia donge nono anapoibuka mshindi katika mashindano ya kitaifa. Aidha michezo huboresha siha ya mchezaji. Fauka ya hayo humwezesha mwanariadha kupata sifa belele na jina zuri kwani jina zuri hung'aa gizani.

Unapotaka kuwa mwanariadha hodari huna budi kuwa na nidhamu ya hali ya juu sana. Ni sharti uepukane na afyuni na anasa zisizofaa. Daima dawamu uzingatie maadili, licha ya hayo, mazoezi kabambe yawe kama ibada kwako vilevile uwaheshimu wakufunzi wako kwani heshima si utumwa.

Ninawasihi kwamba msipotelee michezoni bali pia mzingatie elimu, Elimu ndiyo nguzo ya maisha ya baadaye. Kila mmoja ajifunge kibwebwe na kuuma uzi kila uchao.

Walimu. na wazazi pia nawaomba mshirikiane ili kuwakuza wanafunzi hawa vyema kila mmoja awajibikie kazi yake bila kumwachia yeyote majukumu yote. Watoto hawa ndio viongozi na ni lazima tuwe kielelezo chema kwao.

Ningependa kulikunja jamvi kwa kuwaomba wanariadha wote kujifunga nira ili, kuendeleza sifa ya shule hii na taifa kwa jumla. Mfahamu ya kwamba ninyi ndinyi wabeba mwenge.

Asanteni na Mola awabariki.

---

**31.** Hotuba hii ilitolewa wakati gani?
A. Asubuhi B. Mchana
C. Jioni D. Usiku

**32.** Mtu anayehutubia watu au hadhira huitwaje?
A. Hatibu B. Katibu
C. Hadhara D. Mhutubiaji

**33.** Hotuba hii iliwalenga nani hasa?
A. Walimu B. Wazazi
C. Wanariadha D. Wanafunzi

**34.** Kulingana na taarifa hii, nani ndiye alikuwa mgeni wa heshima?
A. Mkuu wa elimu
B. Mwalimu mkuu
C. Wanariadha
D. Kinara wa kamati ya shule

**35.** Neno afyuni limetumika. Maana yake ni
A. afya
B. hasira
C. heshima
D. kitu kinacholewesha

**36.** Michezo ya riadha ina faida anuwai isipokuwa
A. dongomea B. sifa belele
C. kukosa nidhamu D. huboresha siha

**37.** Ni ushauri gani uliotolewa kwa walimu na wanafunzi?
A. Nidhamu
B. Kuzihgatia maadili
C. Kushirikiana na kutekeleza wajibu wao ipasavyo.
C. kusoma kwa bidii

**38.** Maana ya semi kukunja jamvi kama ilivyotumika katika taarifa hii ni
A. kuandaa jamvi
B. kuwashukuru walio hudhuria
C. kukamilisha mazungumzo
D. kuondoka

**39.** Ni kwa nini walimu na wazazi wanastahili kuwa kielelezo cha watoto wao? Kwa sababu watoto;
A. ni wadogo sana.
B. wanafaa kuwa mwerevu.
C. huiga sana mifano waliyo nayo.
D. watakuwa watu wakubwa.

**40.** Mada ifaayo taaarifa hii ni
A. Hotuba kwa wanariadha
B. Wanariadha
C. Afisa mkuu wa elimu
D. Wazazi na walimu

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 41 - 50;**

Hapo zamani za mababu zetu katika kijiji cha Katani kulikua vijana wawili pacha. Wao walifanana kama shilingi kwa ya pili. Kulingana na desturi za wakamba, vijana hawa walipewa majina ya watu wa ukoo wao ambao walikuwa washaaga dunia. Mmoja aliitwa Mutiso na mwingine Mutuku.

Siku moja Mutiso na Mutuku walipokuwa wamelala mama yao alikwenda mtoni kuteka maji. Walishikwa na usingizi wakalala fofofo. Katika usingizi watoto waliota ndoto ambapo waliona jitu likiwanyemelea huku likiwapigia kelele. Hapo waligutuka kwa pamoja na kweli walisikia kelele zikitoka kila upande. Katika hali hii ya hofu kubwa, walivuka kutoka kitandani na kujificha darini, mara kelele zikatokomea.

Mama alijikaza kisabuni ili afike nyumbani akihofia kuwa wanawe wanatishika na mlio wa ngurumo za radi na mvua iliyokuwa ikinyesha. Alipofika nyumbani alizokuta ni tandiko tu zilizokuwa zimetupwa ovyo ovyo kitandani. Aliwatafuta watoto wake kila mahali lakini hakuwapata. Akadhani labda walienda kwa majirani. Hivyo basi akaamua kutayarisha uji wa mawele halafu atoke nje kuwatafuta. Aliacha uji ukiendelea kuiva motoni na kuenda moja kwa moja kuwatafuta kwa majirani.

Wakati huo huo Mutiso na Mutuku walizidi kupata usingizi wa pono huku juu darini. Kwa bahati mbaya wakaanguka chubwi ndani ya uji kusikia uji unazidi kupata moto Mutiso na Mutuku walianza kutafutana kwa kuitana Mutiso! Mutuku! Mutiso! Mutuku! ili watoke ujini walisichomeke ndiposa kufikia leo ndugu wawili hawa husikika wakiitana Mutiso! Mutuku! Mutiso! Mutuku! kila wakati uji ukipata moto.

**41.** Mutiso na Mutuku walikuwa __________.
A. hawafanani
B. wengi kwenye familia
C. pacha
D. wajinga sana

**42.** Ni neno lipi halina maana sawa na *'kuaga dunia'*?
A. Kufa B. Enda jongomeo
C. Kata kamba D. Kuzaliwa

**43.** Kulingana na hadithi hii unafikiri ni nini Mutiso na Mutuku waliita jitu?
A. Radi B. Jirani
C. Mbwamwitu D. Mwenda wazimu

**44.** Kwa nini mama Mutiso na Mutuku alikazana kukumbilia nyumbani wakati alitoka mtoni?
A. Hakutaka watoto wachukuliwe na jitu
B. Hakutaka kunyeshewa na mvua
C. Alitaka kufika ili awatulize watoto wasishtuke
D. Alitaka kufika kabla watoto kuchukuliwa na majirani

**45.** Waliposikia wakikemewa na kupigiwa kelele Mutiso na Mutuku walikimbilia darini ili?
A. Wasianguke kutoka kitandani kwa uoga
B. Wasichukuliwe na jitu
C. Wasionekane na mama yao anaporudi
D. Wapigie jitu mayowe wakiwa juu darini

**46.** Mama Mutiso na Mutuku alikuwa kutayalisha uji ili
A. aje kuwalisha baada ya kuwapata
B. apate nguvu na kuwaadhibu akiwapata
C. anywe na kupata nguvu ya kuwatafuta
D. awalishe kisha arudi mtoni

**47.** Kulingana na hadithi hii ni wakati gani mama Mutiso na Mutuku alikwenda kuteka maji?
A. Adhuhuri B. Usiku
C. Asubuhi na mapema D. Mchana

**48.** Kuanguka chubwi, kulala fofofo kisanifu ni
A. tanakali za sauti B. methali
C. vitendawili D. semi

**49.** Hadithi hii inaeleza sababu ya ________.
A. mama watoto kutayarishia uji wanawe
B. Mutiso na Mutuku kuanguka chubwi
C. watoto kuota ndoto wanapolala
D. uji kutoa sauti ya Mutiso na Mutuku

**50.** Funzo tunalopata kutokana na hadithi hii ni ___
A. Watoto hupenda kuota wakiwa peke yao
B. Ni vizuri kuwaacha watoto peke yao
C. Usifanye kazi yoyote ukiwa na watoto nyumbani
D. Si vizuri kuwaacha watoto peke yao